

Sauti za ndege asubuhi Le chant des oiseaux le matin



LIDA Portugal ✎
Vilius Aistis Vilimas 🗉
Jacob Haule 🗉 5
Kiswahili! / français / fr



LIDA Stories


lidastories.net

Sauti za ndege asubuhi / Le chant des oiseaux le matin

LIDA Portugal ✎

Vilius Aistis Vilimas 🗉

Jacob Haule (sw), Zina (fr) 🗉



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0).
<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0>



Yulia, mume wake, na binti yao mdogo walikuwa wakiishi katika kijiji kidogo chenye ukimya nchini Ukraini. Yulia alipenda kuamshwa na sauti za ndege kila siku. Hakuwahi kufikiria kuwa angekuja kuishi mbali na nyumbani au kutoamshwa na sauti za ndege asubuhi.

...

Yulia, son mari, et leur petite fille vivaient dans un petit village paisible en Ukraine. Yulia aimait être réveillée chaque matin par le chant des oiseaux. Elle n'a jamais pensé qu'elle vivrait loin de chez elle, ou qu'elle ne serait pas réveillée par le chant des oiseaux le matin.



Mume wake, kwa upande mwingine, alikuwa
akilalamika sana kuwa hana pesa ya kutosha na
akaanza kunywa pombe vibaya. Wakamua
kujaribu bahati yao Ureno. Labda huko
wangepweza kupata pesa zaidi za kujenga
nyumba na wakaiandalia familia yao maisha
mazuri ya baadaye.

...

Son mari se plaignait toujours de ne pas avoir
assez d'argent et a commencé à boire
beaucoup. Ils ont décidé de tenter leur chance
au Portugal. Peut-être que là-bas, ils pourraient
gagner plus d'argent pour construire une
maison et un meilleur avenir pour leur famille.



Yulia alizoea vizuri makazi yake mapya na alianza kufanya kazi kama mfanyakazi wa usafi. Wateja wake walimpenda sana kwa jinsi alivyofanya kazi kwa bidii na heshima yake. Kwa upande mwingine, mume wake alijihisi anatengwa zaidi na zaidi. Kwa sababu ya tatizo lake la ulevi, waajiri hawakuwa na imani naye na hawakutaka kumpa kazi.

...

Yulia s'est bien adaptée à son nouveau chez-elle, et elle a commencé à travailler en tant que femme de ménage. Ses clients appréciaient beaucoup son dur labeur et sa politesse. Son mari, en revanche, se sentait de plus en plus isolé. À cause de son problème d'alcool, les employeurs ne lui faisaient pas confiance et ne lui donnaient pas de travail.



Yulia akaenda katika makazi ya wanawake ambapo alijihisi salama kuliko alivyokuwa kwa muda mrefu. Hakuwahi kujisikia hivyo tangu alipoamshwa na sauti za ndege asubuhi.

...

Yulia est allée à un foyer pour femmes, où elle se sentait plus en sécurité qu'elle ne l'avait été depuis un long moment. Elle ne s'était pas sentie ainsi depuis qu'elle se faisait réveiller par le chant des oiseaux le matin.



Siku moja, alianza kumgomba Yulia. Kisha, akaanza kumsukuma. Kelele na vipigo vikafikia hatua mbaya, hasa akiwa amelewa. Yulia aliogopa na aliingwa na wasiwasi kuhusu binti yake lakini hakuwa na la kufanya.

...

Un jour, il a commencé à crier sur Yulia. Puis, il a commencé à la pousser. Les cris et les coups ont empiré, surtout lorsqu'il était saoul. Yulia avait peur pour elle et pour sa fille, mais elle ne savait pas quoi faire.



Hatimaye, wakati Yulia alilazimika kwenda kwenye chumba cha dharura akiwa amevunjika mkono, walimwambia kuwa unyanyasaji wa majumbani ni tatizo kubwa nchini Ureno. Pia walisema kwamba ilikuwa ni kosa na anapaswa kuripoti polisi.

...

Quand Yulia a finalement dû aller aux urgences à l'hôpital avec un bras cassé, ils lui ont dit que les violences conjugales sont un gros problème au Portugal. Ils ont également dit que c'était un crime et qu'elle devrait porter plainte.



Yulia alikuwa amechoka na hakutaka binti yake mdogo kukua katika mazingira ambayo anashuhudia unyanyasaji kila siku. Yulia alitambua kuwa viashiria vya unyanyasaji vilishakuwepo tangu kitambo hata kama vilikuwa vya namna tofauti.

...

Yulia était épuisée et ne voulait pas que sa fille grandisse dans un foyer où elle voyait de la violence tous les jours. Yulia a réalisé que les signes de maltraitance avaient toujours été là, même s'ils ont pris plusieurs formes différentes.